# MWONGOZO WA KUSHIRIKI KATIKA KAMBI MAALUM YA MAARIFA (BOOTCAMP) KWA AJILI YA MAANDALIZI YA KUJIUNGA NA VYUO VIKUU BORA DUNIANI KATIKA FANI ZA SAYANSI YA DATA, AKILI UNDE, NA SAYANSI SHIRIKISHI KWA MWAKA 2025/2026 (SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+)

## 1. MUHTASARI WA PROGRAMU

| | |
|---|---|
| **Mahali ilipo kambi:** | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha |
| **Tarehe ya kufika kambini:** | Septemba 14, 2025, kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 4 usiku |
| **Tarehe ya kuanza:** | Septemba 15, 2025 |
| **Tarehe ya kumaliza:** | Juni 30, 2026 |
| **Muda wa kambi:** | Wiki 43 |
| **Mapumziko:** | Wiki ya 15 , kuanzia Disemba, 20 2025 hadi Januari 04, 2026), |

## 2. VITU VYA KUBEBA UNAPOKUJA KAMBINI

i) Shuka mbili
ii) Blanketi moja
iii) Taulo
iv) Nguo: za kawaida, rasmi, michezo na za kuzuia baridi kama makoti na masweta kulingana na hali ya hewa ya Arusha.
v) Viatu: viatu vya kawaida, viatu vya michezo/mazoezi, na kandambili (slippers)
vi) Sabuni, mswaki na mafuta ya kujipaka
vii) Pasi ya kunyooshea nguo
viii) Vifaa vingine vya binafsi utakavyohitaji kwa matumizi ya kila siku (mfano dawa binafsi nk.)
ix) Bima ya afya (kwa wenye nayo)
x) Pasipoti (kwa wenye nayo)
xi) Nyaraka muhimu kwa ajili ya maombi ya pasipoti na ufadhili wa masomo: Ushahidi wa Uraia kwa mshiriki na mzazi (cheti cha kuzaliwa au kiapo cha kuzaliwa), kitambulisho cha taifa kilichotolewa na NIDA, picha kwa ajili ya pasipoti
xii) Nakala za vyeti vya elimu

## 3. HUDUMA MBALIMBALI NA MIUNDO MBINU KAMBINI

i) Malazi ambayo yameshalipiwa tayari yaliyojumuisha kitanda, godoro, chandarua na mto.
ii) Posho ya kila mwezi kwa mujibu wa miongozo ya bodi ya mikopo.
iii) Posho ya vifaa vya kuandikia kwa mujibu wa miongozo ya bodi ya mikopo.
iv) Kompyuta mpakato (laptop)
v) Migahawa ya Taasisi (washiriki watajinunulia chakula wenyewe kwa fedha ya posho itakayotolewa na ufadhili huu)
vi) Kumbi za mihadhara
vii) Maabara ya kompyuta
viii) Maktaba
ix) Kituo cha ubunifu na ukuzaji wa mawazo
x) Vitengo vya afya na ushauri nasaha
xi) Uchunguzi wa kiafya kwa ajili ya maandalizi ya safari ya nje ya nchi
xii) Viwanja vya michezo na burudani
xiii) Utambulisho wa walezi wa washiriki wanaume na wanawake

## 4. MAANDALIZI YA KUSAFIRI NJE YA NCHI NA MAFUNZO

i) **Kipindi cha maombi:** kitahusisha maombi ya pasipoti ya kusafiria, pamoja na maombi ya udahili na ufadhili wa masomo katika vyuo vikuu mbalimbali duniani.

ii) **Kozi za kiufundi:** misingi ya matumizi ya kompyuta, utangulizi wa upangaji programu kwa python na R, utangulizi wa hisabati na takwimu kwa sayansi ya data, misingi ya sayansi ya data, kujifunza kwa mashine na akili unde.


iii) **Kazimradi ya mwisho**: Washiriki wataandaa na kuwasilisha miradi ya ubunifu ikiwemo mifano ya suluhisho za akili unde, uthibitishaji na maendeleo endelevu pamoja na kuhitimisha.

iv) **Vyeti vya kitaalamu vya kimataifa**: washiriki wataandaliwa kufanya mitihani na kupata vyeti vinavyotolewa na taasisi mashuhuri zinazotambulika kimataifa kama vile IBM, ISC na WS.

v) **Kozi za maandalizi ya kusafiri na kuishi ugenini**: zikujumuisha ujuzi wa kijamii, mawasiliano, usalama, matumizi ya fedha, ubunifu, kuheshimu taratibu za nchi za watu afya na uzalendo, pamoja na maandalizi ya kufanya mitihani ya kiingereza ya kimataifa.

## 5. NAMNA YA KUFIKA KAMBINI

Kambi maalum ya maarifa ipo katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, iliyopo eneo la Tengeru Arusha. Njia kuu za usafiri wa kufika kambini ni pamoja mabasi ya abiria, uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), na uwanja wa ndege wa Arusha.




## 6. MAWASILIANO

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana

i) **Prof. Liliane Pasape** kwa barua pepe **liliane.pasape@nm-aist.ac.tz** na namba ya simu **0754 36 46 75.**

ii) **Dr. Devotha Nyambo** kwa barua pepe **devotha.nyambo@nm-aist.ac.tz** na namba ya simu **0752 90 51 66.**